

**HOTUBA YA MHESHIMIWA ASSUMPTER N.MSHAMA MKUU WA
WILAYA YA KIBAHA KATIKA SIKU YA MLIPA KODI TAREHE 20
OKTOBA, 2017 HALMASHAURI YA MJI KIBAHA**

Mhe. Leonard S. Mlowe
Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Kibaha,

Mhe. Silvestry F. Koka (MB)
Mbunge wa Jimbo la Kibaha Mjini,

Wahe. Madiwani,

Ndugu Sozi Ngate
Katibu Tawala Wilaya ya Kibaha,

Ndugu. Jenifa C. Omolo
Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kibaha,

Viongozi wa Vyama vya Kisiasa,

Wakuu wa Idara na Vitengo,

Walipa Kodi wote,

Waandishi wa habari,

Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana,

Napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sote kuwa hapa siku ya leo. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kibaha na Kamati yake ya Maandalizi kwa kunialika ili niwe mgeni rasmi katika maadhimisho ya siku ya mlipa kodi katika Halmashauri yenu.

Mnenipa heshima kubwa na nimefarijika sana kujumuika nanyi katika hafla hii ambayo hutoa fursa kwa mlipakodi na mkusanyaji kushirikiana

katika kutathmini mafanikio na changamoto zilizopo katika kukusanya mapato ya Halmashauri na kuweka mikakati bora zaidi ya kuweza kufanikisha zoezi zima la kukusanya kodi kwa utaratibu wa uwazi unaokubalika kwa maendeleo ya Halmashauri ya Mji wetu wa Kibaha.

Ndugu walipakodi na wageni waalikwa,

Kama ilivyokwisha zungumzwa kuwa leo ni Siku ya Mlipakodi, hatuna budi kuadhimisha siku hii kwa kutambua kuwa mlipakodi ni mdau muhimu kwa maendeleo ya Halmashauri ya Mji wa Kibaha na Taifa kwa ujumla. Ni wakati muafaka wa kutafakari na kujiuliza kama huduma stahiki ambazo mlipakodi anatakiwa kupata kutohana na kodi yake anazipata.

Aidha, ni wakati wa kuangalia kwa undani changamoto zilizopo katika uhusiano baina ya mlipakodi na Halmashauri katika kutekeleza wajibu wa kukusanya kodi ili kuzirekebisha na kuwezesha ulipaji kodi kwa hiyari na wakati stahili. Siku ya mlipakodi ni fursa muhimu kwa sisi sote kushirikiana pamoja katika kuangalia mfumo mzima wa ulipaji kodi ili kuondoa mapungufu na kuimarisha uzalendo wa kweli na uwajibikaji kwa wadau wote katika kukusanya mapato.

Aidha, kwenye Taarifa yenu nimesikia kuwa Halmashauri ya Mji Kibaha imeweza kupata **TUZO YA UBORA** inayotolewa na **BODI YA WAHASIBU NA WAKAGUZI WA HESABU TANZANIA** (NBAA) ya ufungaji wa Hesabu kwa kuzingatia Sheria za Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 kwa kushika nambari 1 kati ya Halmashauri 188. Mimi Kama Mkuu wenu wa Wilaya niseme wazi kuwa nimefarijika sana kwa kazi nzuri tena yenyе heshima kubwa kwa Halmashauri yenu mliyoionesh. Tunapoelekea kwenye uchumi wa Kati ifikapo 2020, Rais wetu mpandwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli anatamani kila

Halmashauri iwe na Watendaji wachapakazi,Wabunifu na wanaotumia Maarifa yao kwenye kazi kama hawa waliotufungia Mahesabu. Mimi naamini kwa kazi hii nzuri mliyoifanya Mwenyezi Mungu atawalipa. Hongereni sana!

Ndugu walipakodi na wageni waalikwa,

Tunapoadhimisha siku ya mlipakodi, ni dhahiri tunaongelea mafanikio na changamoto tulizozipata kwa kipindi kilichopita. Vilevile, ni dhahiri kwamba kwenye mafanikio ni jambo jema sana kujipongeza, na kwenye changamoto ni wakati mzuri wa kuangalia namna ya kukabiliana nazo. Ni kweli yapo mafanikio ambayo yamepatikana katika sekta ya kodi. Moja ya mafanikio yaliyopatikana ni kuongezeka kwa mapato ya Halmashauri kupitia vyanzo vyake vya ndani. Na mapato yanapoongezeka ni dhahiri kuwa ninyi walipakodi mlilipa kwa wakati tena kwa kujitoa mkitambua kuwa maendeleo siku zote yanategemea kodi zetu. Hongereni sana!

Takwimu zinaonyesha kwamba mapato yanayotokanayo na vyanzo vya ndani vya Halmashauri yameongezeka kutoka shilingi 2,560,091,596.00 kwa mwaka wa fedha 2012/2013 hadi kufikia shilingi 3,954,400,000 kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Ndugu walipakodi na wageni waalikwa,

Takwimu hizi zinatuonyesha kuwa mapato yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka, lakini ukweli ni kwamba ongezeko hili bado halikidhi mahitaji ya Halmashauri katika kuwalettea wananchi maendeleo ya haraka na kwa kasi inayotarajiwa na wananchi waliowengi hasa ukizingatia kuwa Uongozi wa awamu ya tano chini Rais wetu Mhe. Dkt John Pombe Joseph Magufuli pamoja na kuwa na *falsafa ya hapa ni kazi tu*, lakini pia unasisitiza kutoa au kudai risiti unapouza ama kununua

bidhaa. Unapotoa ama kudai risiti utakua umetimiza wajibu wako wa kulipa kodi.

Aidha, Kitendo hiki cha kulipa kodi kwa wakati na Halmashauri kuzielekeza kwenye Miradi ya Maendeleo, hakika mmemuunga Mkono Mheshimiwa Rais kwa vitendo kwa kuwaletea wananchi Maendeleo.

Napenda kutoa msisitizo kwa Halmashauri kuhakikisha kuwa inaongeza ukusanyaji wa mapato hasa kuendelea kubuni vyanzo vipyta vya Mapato ili kukidhi mahitaji ya kuwashudumia wananchi. Kwa kufanya hivyo Halmashauri itaachana na utegemezi kutoka Serikali Kuu na Wahisani ambao misaada yao mara nyingine haifiki kwa wakati na kuathiri utekelezaji wa mipango iliyopo. Rai yangu kwenu walipa kodi, nawaombeni mzidi kutoa ushirikiano wa dhati kwa Halmashauri yenu.

Ndugu walipakodi na wageni waalikwa,

Leo tunatoa vyeti kwa makundi mbalimbali ya walipakodi ambapo kundi la kwanza ni lile la wale ambao wameonyesha uadilifu mkubwa katika kulipa kodi kwa hiari na hivyo kuchangia juhudzi za Halmashauri ya Mji Kibaha za kupambana na umaskini. Aidha, kuna kundi la walipakodi hodari ambalo linajumuisha Makampuni, Taasisi na Watu binafsi, hali kadhalika kundi la wahamasishaji na wafuatiliaji wa makusanyo ya mapato ambalo linahusisha na Waheshimiwa Madiwani wa Kamati ya Fedha na Utawala kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na Watumishi wa Halmashauri ya Mji Kibaha. Nawapongeza sana wale wote waliotunukiwa vyeti hivyo kwa kazi nzuri mliyoifanya na naamini kuwa vyeti hivyo vitakua motisha ya kufanya vizuri zaidi siku za usoni. Lengo kubwa n La Mapato haya ni kutoa huduma kwa wananchi na kuwaletea Maendeleo.

Tunapohitimisha siku hii ya mlipakodi ndipo tunaanza maandalizi ya siku nyingine ya mlipakodi. Naamini mliopewa vyeti vya kufanya vizuri

mnaondoka leo hapa na hamasa ya kufanya vizuri zaidi, ili mwakani mje tena kutunukiwa vyeti vya mafanikio. Na wale ambao hawakupata vyeti leo naamini nao watamotishwa na kufanya vizuri zaidi ili mwakani nao wawemo kwenye makundi ya watakaotunukiwa vyeti.

Ndugu walipakodi na wageni waalikwa,

Sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa namba 9 ya mwaka 1982 (Local Govt. Finance Act. No. 9 of 1982 CAP 290) imeipa Halmashauri uwezo wa kukusanya mapato kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali ikiwa na lengo la kuiwezesha Halmashauri kutoa huduma stahiki kwa wananchi wake. Halmashauri inapaswa kupiga vita kwa nguvu zote aina yoyote ile ya rushwa, ukwepaji kodi na kutoa adhabu kali kwa wakwepaji kodi. Aidha, kuendelea kutoa elimu ya kodi ili kuongeza uelewa kwa baadhi ya walipa kodi juu ya malengo na matumizi sahihi ya kodi inayokusanywa. Naomba niwakumbushe tena kudai na kutoa za stakabadhi mara zote kwenye biashara zenu, kutokufanya hivyo ni kosa kisheria na inapogundulika unaweza kufikishwa kwenye vyombo vya dola.

Nimesikia taarifa yenu kuhusu uimarishaji wa matumizi ya mifumo ya kompyuta katika ukusanyaji wa kodi ili kupambana na tatizo hili na kuifanya Halmashauri yenu kuwa na mbinu ya kisasa ya usimamizi wa kodi na kujenga usimamizi wa kodi shirikishi. Aidha, muendelee kuimarisha mahusiano yenu na taasisi mbalimbali za Serikali kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), SUMATRA, TANROAD, TANESCO, TAKUKURU, Mahakama na Polisi ili kuisaidia Halmashauri katika ukusanyaji wa Mapato kutoka kwa walipa kodi. Naendelea kutoa msisitizo kuwa Mlipakodi na mkusanya kodi wanatakiwa kushirikiana kama wadau muhimu katika sekta ya ukusanyaji kodi hivyo pande zote mbili zihakikishe kuwa zinafanya kazi kwa pamoja.

Ndugu walipakodi na wageni waalikwa,

Kwa maneno haya machache ninapenda kumalizia kwa kutoa pongezi na kutambua umuhimu wa walipakodi wote wa Halmashauri kwa kazi kubwa mnayofanya. Halmashauri ya Mji Kibaha inatambua umuhimu wenu kwa Maendeleo ya nchi yetu. Nawapongeza wote walioshiriki kuandaa maadhimisho haya, wito wangu kwenu msirudi nyuma. Endelezeni juhudi za kutoa elimu ya kodi kwa walipa kodi wote na wanachi kwa ujumla ili kujenga uelewa wa pamoja juu ya umuhimu wa ulipaji kodi kwa hiyari na kwa wakati.

Mtambue kwamba mna kazi kubwa ya kutimiza azma hii pamoja na kujenga uwezo zaidi wa kuongeza makusanyo ili kuendelea kugharamia sehemu ya miradi ya maendeleo kutokana na vyanzo vya ndani. Changamoto iliyoko mbele yenu ni kuimarisha mafanikio yaliyopatikana na kuyaboresha zaidi. Lengo letu sote liwe ni kulipa kodi kwa hiari; kukusanya kodi kwa kutumia kanuni, sheria na taratibu ili kuongeza mapato na hivyo kuendelea kutoa huduma bora na endelevu kwa maendeleo ya wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha.

"TIMIZA WAJIBU, LIPA KODI KWA MAENDELEO YAKO"

Mungu ibariki Kibaha,
Mungu ubariki Mkoa wa Pwani
Mungu Ibariki Tanzania
Mungu Ibariki Afrika

Ahsanteni kwa kunisikiliza!